GAZETI LA KWANZA LA ISLAM KUTOLEWA KWA LUGHA YA KISWAHILI - MWAKA 1936

AHMADIYYA MUSLIM JAMAAT TANZANIA

Mapenzi Yangu

MAPENZI KWA WOTE BILA CHUKI KWA YEYOTE

JUZU NO. 238 **Shawwal-Qa'dah** 1445 **AH** **Mei–** 2024 **Hijrat** 1403 **HS** **BEI TSH 800/=**

* Matukio kutoka kwa Maisha ya Mtukufu Mtume saw

Kuwakumbuka Mashahidi wa Uhud

Baada ya kusoma Tashahhud , Ta'awwuz na Surah al-Fatihah , Khalifa Mtukufu, Hazrat Mirza Masroor Ahmad (atba) alisema:

Kabla ya Ramadhani, hapo awali nilikuwa nikijadili safari mbalimbali za Mtukufu Mtume (saw) . Leo nitaendelea kutaja jambo hili.

Khalifa Mtukufu (atba) alisema kwamba mama yake Hadhrat bin Mu'adh (ra) alikwenda kwa Mtukufu Mtume (saw) akiwa amekaa juu ya farasi wake. Mtukufu Mtume (saw) alisimama kwa ajili yake na kumjulisha kuhusu kifo cha kishahidi cha mwanawe Hazrat Amr bin Mu'adh (ra) . Kwa kujibu, alisema kwamba kumuona Mtukufu Mtume (saw) akiwa salama na mwenye afya njema, wasiwasi wake wote ulipungua. Mtukufu Mtume (saw) alimpa bishara njema kwamba mashahidi wote wa Uhud walikuwa pamoja Peponi na wameziombea familia



Muhtasari wa hotuba ya Ijumaa ya Hadhrat Khalifatul Masih Vatba ilitolewa Tarehe 12 APRILI 2024

zao. Alimuagiza kufikisha hili kwenye nyumba zote za mashahidi. Mtukufu Mtume (saw) kisha akawaombea mashahidi wote na familia zao.

Khalifa Mtukufu (atba) alisema kwamba Hadhrat Musleh Maud (ra) alikuwa akiwahutubia wanawake wa Ahmadiyya na akasema kwamba hao walikuwa ni masahaba wa kike wakati wa Mtukufu Mtume (saw) ambao walikuwa mstari wa mbele pamoja na masahaba wa kiume katika kueneza ujumbe wa Uislamu. Ulimwengu wa Kiislamu unajivunia kujitolea kwao, na kwa vile ni madai yako ya kumwamini Masihi Aliyeahidiwa (as) , wewe ni kielelezo cha masahaba wa kike wa Mtukufu Mtume (saw) . Alisema hata hivyo lazima wachambue ikiwa wana shauku, bidii na mwanga sawa na wao. Dhabihu zao zilipendwa sana na Mungu Mwenyezi hivi kwamba yale waliyoyapata ndani ya miaka michache hayakuweza kufikiwa kwa karne nyingi na mataifa mengine mengi.

Khalifa Mtukufu (atba) alisema kwamba alikwishataja matukio fulani hapo kabla, lakini wakati fulani, wakati wa kuyasoma

SEMINA YA AMILA ANSARULLAH YAFANA

KUSINI MWA JANGWA LA SAHARA

Na Mwandishi Wetu.



Kwa msaada mkubwa wa Allah na rehema zake mkutano wa kimataifa wa AMILA ANSWARULAH uliofanyika Masjid Salaam toka tarehe 20 April 2024 hadi 21 April 2024 chini ya Katibu wa Huzur anayeshughulika na Answarullah ABDULKHALEQUE TALUKDAR SAHIB na kufunguliwa na Amir na Mbashiri mkuu wa Tanzania SHEIKH TAHIR MAHMOOD CHAUDHRY SAHIB. Wajumbe waliohudhuria ni kutoka Tanzania, Malawi, Uganda, Kenya, Zambia, Zimbabwe, Cameroon, South Africa, Afrika ya kati na Jamhuri ya kidemokrasia ya Congo.

Semina ilianza kwa usomaji wa Kuruani Tukufu na tafsiri kufanyika katika lugha za kiingereza na kifaransa. Baada ya hapa Amir na Mbashiri Mkuu aliwaongoza wana semina katika maombi ya kimya. Sadr Answarullah Dr. SWALEH K PAZI alisimama na kusoma ahadi ya Answarullah iliyokuwa inarudiwa na wote waliohudhuria semina. DR. PAZI alimuomba Amir na Mbashiri mkuu atoe

UK. 04

JIFUNZE KUISOMA NA KUIELEWA BIBLIA UK. 07

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

W a j i b u W e t u

Watafiti na wasomi w a n a o j i s h u g h u l i s h a kuelewa dini tukufu ya Islam, wameanza kwa kupitia vitabu vya Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya kuelewa kwa kiwango fulani mafundisho sahihi ya dini tukufu ya Islam ambayo imeletwa kumkomboa biandamu katika maana pana ya dhana hiyo ya ukombozi.

Kitabu kimoja maarufu kilichotolewa na UNESCO ambacho kinaelezea historia ya Afrika *'General History of Africa Vol. III, Africa from the Seventh to the Eleventh Century'* kilichoandikwa na M. Elfast kwenye ukurasa wa 46 ameeleza ya kwamba; Neno 'Jihad' halina uhusiano wowote na vita takatifu. Neno hili linatokana na neno 'JAHADA' ambalo maana yake ni kufanya jitahada. Muandishi huyo anatoa mfano kwa maneno ya Mtume Mtukufu[saw] pale alipowaambia Masahaba Zake pindi walipokuwa wakirejea kutoka kwenye vita fulani aliposema; 'tumetoka kwenye jihadi ndogo kuelekea kwenye jihadi kubwa' ambapo masahaba zake walipomuuliza hiyo jihadi kubwa ni ipi, yeye Mtukufu Mtume Muhammad[saw]aliwaambia; Jihadi kubwa zaidi ni jihadi ya kuitakasa nafsi'.

Kwa kweli vita yoyote iliyopiganwa na Mtume Mtukufu[saw] ilikuwa ni kujilinda tu dhidi ya maangamizi ya Islam kutoka kwa wapinzani wa dini tukufu ya Islam ambao walidhamiria kunyanyua upanga kuifutilia mbali Islam kwa kutaka kumuu Mtume Mtukufu[saw] na Masahaba zake.

Msomi mwingine maarufu ambaye ni Profesa wa chuo kikuu cha Oxford nchini Uingereza Bw. John L. Esposito kwenye kitabu chake cha ***'Islam the straight path'*** ukurasa wa 16 amefutilia mbali kashfa zote anazosingiziwa Mtukufu Mtume[saw] kuhusiana na kuoa wake wengi; Msomi huyo kwenye kitabu chake hicho anasema; Lawama zote hizo dhidi ya Mtukufu Mtume Muhamamd[saw] sio sahihi hata kidogo, anatoa mfano mmoja wa kuzingatiwa, ikikumbukwa kwenye historia yake Mtume Mtukufu[saw] kwenye ujana wake mzima ambapo ndipo nguvu ya matamanio huwa kubwa, yeye alimuoa na kuishi na mke mmoja tu mzee (Bi. Khadija) ambaye aliishi naye hadi kufa kwake. Ingewezekanaje kwa mwanaume kijana wa miaka 25 kustahamili kwa ujana wake kuwa na mke mmoja tena mzee kwa kipindi kichote hicho? Lakini pia anajenga hoja kutoka kwenye Biblia tunaona akina Abraham, Daud n.k wameoa wake wengi na hatuoni wakikashifiwa kwa tendo hilo hilo moja, ambapo ukweli tunaona kuwa Mtume Mtukufu[saw] alilazimika kuoa wake wengi mwishoni mwa umri wake ambapo ikitazamwa kwa jicho la adili, itabainika wazi kuwa shabaha ya ndoa hizo ilikuwa ni ama kurahisisha mafundisho ya Islam yawafikie wanawake kwa njia rahisi kupitia wakeze, ama vilevile dhamira kuwahifadhi wake hao ambao wengi wao walikuwa ni wajane.

Taswira hiyo tunayoipata hapo juu inatuonyesha kuwa tunayo hazina kubwa iliyofichika kwenye vitabu vyetu vya Jamaat. Kwani kama wasomi hao hapo juu wasingepata kusoma vitabu vya Jamaat wasingeweza kutoa utetezi huo mzuri kwa mtukufu mtume[saw] na Islam kwa ujumla.

Hivyo tukiwa Waahmadiyya tunao wajibu mkubwa wa kuhakikisha kuwa hazina tuliyo nayo inafikishwa kwa watu wengi kadri iwezekanavyo. Kwa mathalani ukiwa mwanafunzi wa chuo unao wajibu wa kuhakikisha vitabu vyetu vinawafikia wanafunzi wa vyuo kwa kufikisha vitabu vya Jamaat kwenye makbtaba za vyuo. Ukiwa mwanasiasa hakikisha unawapatia wanasiana wenzako vitabu vya Jamaat, hata katika ngazi ya kifamilia tunao wajibu wa kuwafikishia vitabu vya Jamaat kwa ndugu zetu ambao sio Waahmadiyya ili nao waweze kunufaika na hazina tuliyo nayo ambapo hatimaye kwa kufanya hivyo tutaweza kufikisha ujumbe wa Masihi Aliyeahidiwa[as] kwa watu wengi zaidi na kuweza kuwaongoza kwenye njia iliyonyyooka, njia iliyo sahihi itakayowaunganisha na Muumba wao. Tunatoa shime kwa kila mwana Jamaat kuhakikisha anafikisha vitabu vya Jamaat kwa watu walio ni wa kada yake ili kusaidia ujumbe wa Masihi Aliyeahidiwa[as] ufike kwa watu wote duniani kote.



QUR'AN TUKUFU

وَعَدَ اللّٰهُ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا مِنْكُمْ وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ
لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْاَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِيْنَ مِنْ
قَبْلِهِمْ ۪ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِيْنَهُمُ الَّذِي ارْتَضٰى لَهُمْ
وَلَيُبَدِّلَنَّهُمْ مِّنْۢ بَعْدِ خَوْفِهِمْ اَمْنًا ؕ يَعْبُدُوْنَنِيْ
لَا يُشْرِكُوْنَ بِيْ شَيْـًٔا ؕ وَمَنْ كَفَرَ بَعْدَ ذٰلِكَ فَاُولٰٓئِكَ
هُمُ الْفٰسِقُوْنَ ۝

56. Mwenyezi Mungu Amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu na kufanya vitendo vizuri, bila shaka Atawafanya makhalifa katika ardhi kama Alivyowafanya makhalifa wale wa kabla yao, na kwa yakini Atawaimarishia dini yao Aliyowapendelea, na Atawabadilishia amani baada ya hofu yao. Wataniabudu, hawatanishirikisha na cho chote. Na atakayekufuru baada ya hayo, basi hao ndio wavunjao amri.

JUZU 18, QAD AFLAHA — 24. SURA AN-NUUR

NUKUU YA HADITHI

Bwana wetu Mtume Mtukufu Muhammad[saw] alisema:

مَا كَانَتِ النُّبُوَّةُ قَطُّ اِلَّاتَبِعَتْهَاخِلَافَةٌ۔

Tafsiri: Hakuna unabii katu ila ukhalifa unaufuata.

(Kanzul Ummal,Al-Faslul Awwal, hadith no.3224)



Nukuu ya Masih Aliyeahidiwa[as]

Imam uz zaman seyedna Ahmad as alisema akieleza jambo hili kwamba: "Maana ya khalifa ni naibu ambaye hujadidisha dini. Wale watu wanaokuja kuliondoa giza linaloenea baada ya kuondoka kwa Manabii, huitwa makhalifa." (Malfuzaat.j.4 uk.383).

Kisha anasema pengine:

"Khalifa anakuwa naibu na naibu wa Mtume kwa maana ya uhakika ni yule tu ambaye anakuwa na sifa zilizokamilika (kama) za Mtume kuwa dhilli(mfano) yake, kwa sababu Mtume saw hakuwaita wafalme wadhalimu kuwa makhalifa kwani khalifa kwa kweli anakuwa mfano yaani dhill wa nabii, na kwa sababu mtu yeyote hawezi kubaki hapa duniani milele, hivyo Mwenyezi Mungu alipenda kwamba manabii ambao ni bora na wema zaidi kuliko watu wote wa

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Dr. Swaleh Kitabu Pazi
Kompyuta: Jabiri Faraji Bishazo.
Mchapishaji: Sheikh Raghib Zia ul Haq
Msambazaji: Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe: 1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Mahmood Hamsin Mubiru.
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.

*_Matukio kutoka kwa Maisha ya Mtukufu Mtume SAW

Kuwakumbuka Mashahidi wa Uhud

Kutoka Uk wa 1..

kutoka pembe nyingine huleta bidii na hamasa maalum ndani ya mtu. Kwa hiyo, Khalifa Mtukufu (atba) alimnukuu Hadhrat Musleh Maud (ra) alipokuwa akizungumzia matukio ya masahaba wa kike wakati wa Mtukufu Mtume (saw) . Alisema kwamba wakati wanawake wa Madina waliposikia habari za kufariki kwa Mtukufu Mtume (saw) , walikimbilia kwenye uwanja wa vita wa Uhud. Wengi wao walihakikishiwa njiani kwamba alikuwa hai na mzima, lakini mwanamke mmoja - ambaye mume wake, kaka na baba yake wote waliuawa - aliendelea kusonga mbele. Aliuliza kuhusu Mtukufu Mtume (saw) mara tu alipowasili. Baada ya kuambiwa kuhusu kifo cha kishahidi cha watu wa familia yake, alitaka tu kusikia kuhusu Mtukufu Mtume (saw). Alipoambiwa kwamba yu hai, alimkimbilia na kusema, 'Ikiwa uko hai na u mzima, hakuna jambo lingine lolote kwangu.' Tazama jinsi alivyokuwa akimpenda Mtukufu Mtume (saw) kwamba mume wake, baba yake na kaka yake wote walikuwa wameuawa kishahidi, lakini jibu lake pekee lilikuwa ni kujua kuhusu Mtukufu Mtume (saw) .

*_Uvumi wa Kifo cha Mtume Wafika Madina_*
Khalifa Mtukufu (atba) amemnukuu Hadhrat Musleh Maud (ra) ambaye aliandika kuhusiana na ushujaa ulioonyeshwa na watu wa Madina:

'Uvumi wa kifo cha Mtume (saw) na habari za kutawanywa kwa jeshi la Waislamu zilifika Madina, kabla ya mabaki ya jeshi la Waislamu kurejea mjini. Wanawake na watoto walikimbia wazimu kuelekea Uhud. Wengi wao walijua ukweli kutoka kwa askari waliokuwa wanarejea na wao wakarudi. Mwanamke mmoja wa kabila la Banu Dinar aliendelea mpaka akafika Uhud. Mwanamke huyu alikuwa amepoteza mume, baba na kaka yake katika vita. Kulingana na wasimulizi wengine, pia alikuwa amepoteza mtoto wa kiume. Askari mmoja aliyekuwa akirudi alikutana naye na kumwambia kwamba baba yake alikuwa amekufa. Akajibu, "Simjali baba yangu; niambie kuhusu Mtume (saw) . "Askari huyo alijua kuwa Mtume (saw) yu hai, hivyo hakujibu swali lake mara moja, bali aliendelea kumwambia kuhusu kaka yake na mume wake ambaye pia alifariki. Katika kila taarifa alibaki bila kuguswa na akauliza tena na tena, "Ni nini amefanya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw)? Ulikuwa usemi wa ajabu kuutumia, lakini tunapokumbuka kuwa ni mwanamke aliyeutumia, hauonekani kuwa wa ajabu tena. Hisia za mwanamke ni kali. Mara nyingi yeye huzungumza kuhusu mtu aliyekufa kana kwamba yuko hai. Ikiwa mtu huyo ni ndugu wa karibu, ana mwelekeo wa kulalamika kwake na kuuliza kwa nini anamtelekeza na kumwacha bila matunzo na wa kumuangalia. Ni kawaida kwa wanawake kuomboleza vifo vya wapendwa wao kwa njia hii. Usemi uliotumiwa na mwanamke huyu, kwa hiyo, ni sahihi kwa mwanamke anayehuzunika kwa kifo cha Mtume (saw). Mwanamke huyu alimpenda Mtume (saw) na alikataa kuamini kuwa amekufa hata baada ya kusikia kuwa amekufa. Wakati huo huo hakukanusha habari hizo bali aliendelea kusema kwa huzuni ya kweli ya mwanamke, "Ni nini amefanya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) ?" Kwa kusema hivi alijifanya Mtume (saw) yu hai, na akalalamika kwamba kiongozi mwaminifu kama yeye amechagua kuwapa maumivu yote ya kutengana. Askari aliyekuwa akirejea alipogundua kwamba mwanamke huyu hajali kifo cha baba yake, kaka yake na mume wake, alielewa undani wa mapenzi yake kwa Mtume (saw) na akamwambia, "Ama kuhusu Mtume (saw) yuko kama unavyotamani, hai kabisa." Yule mwanamke alimuuliza yule askari amuonyeshe Mtume (saw). Alionyesha sehemu moja ya uwanja. Yule mwanamke akakimbilia sehemu hiyo na kumfikia Mtume (saw), akashika vazi lake mkononi, akalibusu kisha akasema "Baba yangu na mama yangu wajitolee kwako ewe Mtume (saw) wa Mwenyezi mungu, ukiishi wewe, sijali atafariki nani". Tunaweza kuona, kwa hiyo, ni ujasiri gani na kujitolea Waislamu - wanaume na wanawake - walionyesha katika vita hivi.

Waandishi wa Kikristo wanasimulia kwa fahari hadithi ya Maria Magdalene na wenzake na kutuambia juu ya kujitolea na ushujaa wao. Inasemekana kwamba katika saa mapema za asubuhi, walipenya baina ya Wayahudi na kuelekea katika kaburi la Yesu (as). Lakini hii ni nini ikilinganishwa na kujitolea kwa mwanamke huyu wa Kiislamu wa kabila la Dinar? Mfano mmoja zaidi umeandikwa katika historia. Baada ya maiti kuzikwa na Mtume (saw) akiwa anarudi Madina, aliona wanawake na watoto waliotoka Madina kuja kumpokea. Kamba ya ngamia wake ilishikwa na Sa'd bin Mu'adh, chifu wa Madina. Hadhrat Sa'd (ra) alikuwa akimuongoza ngamia kwa ufahari. Alionekana kutangaza kwa ulimwengu kwamba Waislamu walikuwa wamefanikiwa baada ya yote kumrudisha Mtume (saw) Madina akiwa salam na furaha. Alipokuwa akisonga mbele alimwona mama yake mwenyewe mzee akisonga mbele kukutana na kundi la Waislamu waliokuwa wakirejea. Mwanamke huyu mzee alikuwa na uwezo dhaifu wa kuona. Hadhrat Sa'd (ra) alimtambua na, akamgeukia Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) akasema: "Huyu, ewe Mtume (saw), ni mama yangu." "mwache aje mbele," akajibu Mtume (saw) . Yule mwanamke alikuja mbele na huku akiangalia kwa uwazi akajaribu kuuona uso wa Mtume (saw). Hatimaye, aliweza kuuona na akafurahi. Mtukufu Mtume (saw) alipomwona akasema, "Ewe Mwanamke, ninahuzunika kwa kufiwa na mwanao". "Lakini," yule mwanamke aliyejitolea akajibu, "Baada ya kukuona ukiwa hai, nimemeza maafa yangu yote." Usemi wa Kiarabu aliotumia ulikuwa "Nimechoma msiba wangu na kuumeza." Je, usemi huu unaonyesha hisia zipi? Kwa kawaida, huzuni humla mwanadamu, na hapa palikuwa na mwanamke mzee ambaye alikuwa amefiwa na mwanawe, fimbo ya uzee wake. Lakini alisema kwamba, badala ya kuruhusu huzuni yake kumtafuna, alikuwa amekula huzuni yake. Ukweli kwamba mtoto wake alikufa kwa ajili ya Mtume (saw) kungemsaidia katika siku zake zote zilizobaki.' (Introduction to the Study of the Holy Qur'an, uk. 145-146)

*_Mazishi ya Mashahidi wa Uhud_*
Akielezea mapenzi ya Mtukufu Mtume (saw) kwa mashahidi wa Uhud, Hazrat Mirza Bashir Ahmad (ra) anaandika:

Ingawa sala ya mazishi haikusaliwa wakati huo, baadaye, karibu na zama za kufariki kwake, Mtukufu Mtume (saw) alisali sala ya jeneza haswa kwa mashahidi wa Uhud, na akawaombea kwa uchungu mkubwa. Mtukufu Mtume (saw) aliwakumbuka mashahidi wa Uhud kwa upendo na heshima maalum.

Wakati mmoja, Mtukufu Mtume (saw) alipopita karibu na makaburi ya mashahidi wa Uhud, alisema, "Hawa ni watu ambao mimi ni shahidi wao juu ya imani yao." Hadhrat Abu Bakr (ra) alijibu, "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Sisi si ndugu zao? Je, sisi pia hatujaukubali Uislamu kama wao? Je, sisi pia hatushiriki katika Jihad kwa ajili ya Mwenyezi Mungu kama walivyoshiriki wao?" Mtukufu Mtume (saw) alisema: "Hakika! Lakini nitajuaje mtakalofanya baada ya kufa kwangu?" Juu ya hili Hadhrat Abu Bakr (ra) alianza kulia, na aliendelea kulia sana. Kisha akasema, "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Je, tutaweza kuishi baada ya kifo chako?"

Masahaba pia waliwaheshimu sana mashahidi wa Uhud, na daima waliweka kumbukumbu ya Uhud hai ndani ya mioyo yao kama tukio takatifu. Kama hivyo, katika tukio moja baada ya kufariki kwa Mtukufu Mtume (saw) , Hadhrat Abdur Rahman bin Auf (ra) aliletewa baadhi ya chakula ili afungue saumu yake, ambacho labda kilitayarishwa kwa ustadi.

Kwa hili, alikumbushwa wakati wa Uhud, wakati Waislamu hawakuwa hata na nguo za kutosha kuwasitiri mashahidi wao, na walikuwa wakikata nyasi kufunika miili yao. Abdur Rahman bin Auf (ra) alifadhaishwa sana na kumbukumbu hii kwamba alianza kulia bila kupumzika na kuondoka bila kula, ingawa alikuwa amefunga.'

(The Life & Character of the Seal of Prophets (sa) - Juzuu ya

UK. 04

SEMINA YA AMILA ANSARULLAH

KUSINI MWA JANGWA LA SAHARA

Kutoka Uk 01..

neno la ufunguzi. SHEIKH CHAUDHARY alitoa shukran kwa Allah kwa kuwezesha wajumbe kutoka sehemu za mbali na karibu kukutana. Alimshukuru Kiongozi wetu Mpendwa Khalifatul Masih wa V (atba) ambaye ameipa heshima Tanzania kwa kuichagua kuwa mwenyeji wa semina hii muhimu. Aliwahakikishia wanasemina kuwa ofisi yake iko wazi na iko tayari kutoa msaada utakaofanikisha semina hiyo.

Hotuba rasmi ya kufungua kikao ilitolewa na Katibu wa Huzur, katika hotuba yake aliwaeleza wanasemina kuwa Huzur anaongozwa na Allah hivyo ni muhimu kuzingatia anayotuagiza na kuyatekeleza hiyo ndiyo njia pekee ya maendeleo yetu na ustawi. Aliwakumbusha wanasemina kuwa silaha pekee tuliyo nayo ni maombi.

Tafadhali jitahidini kumuandikia barua Huzur kwa ajili ya maombi na mwongozo. Lazima tujenge utamaduni wa kumuandikia kwani hili ndio Jambo linalompa furaha. Na Ile ripoti ya Kila miezi mitatu ni muhimu, tukumbuke kuiandika. Ulimwengu kama anavyosema Khalifatul Masih V (atba) hauwezi kubadilishwa isipokuwa kwa silaha ya maombi. Hii ni silaha muhimu na haijawahi kushindwa asilani abadani. Tunayo bahati ya kuwa na Kiongozi anayetuonesha njia na hii inatokea kupitia hotuba zake za Ijumaa, hotuba mbali mbali anazozitoa na kutazama vipindi vinavyorushwa na MTA kwa ujumla. Hakuna kiongozi yeyote mwingine Duniani anayewajali wale anaowaongoza Kama Huzur. Tuna bahati ya kwamba tuna mapenzi yake na haya mapenzi ndiyo tunayoyaona yametapakaa mahali popote walipo Waahmadiyya. Fikra zake zote ni juu ya maendeleo yetu na maendeleo yetu ni kutimiza haki za Allah na alivyoviumba.

Maneno yake haya kwa uzuri zaidi yaligusa juu ya wajibu wa viongozi wa Answarullah kwa mnasaba wa hotuba za Huzur kwa mataifa mbali mbali.

Mara baada ya maneno mazito kutoka kwa katibu wa Huzur, wanasemina waliombwa watoe maoni yao, maswali au mchango wowote ule. Mjumbe kutoka Kenya alieleza shughuli zinazofanywa na Answarullah. Kalenda ya matukio na wanajitahidi kuitekeleza. Kwa sababu Islam haishughuliki na roho peke yake bali pia mwili, matibabu kupitia kambi yanatolewa mara kwa mara kwa wale ambao hawajiwezi huwasaidia.kwa hivi sasa Tanzim iko mbioni katika kukamilisha Tajneed ya Answarullah.

Mjumbe kutoka Uganda alieleza wanalokumbana nalo kuhusu wanafunzi. Ratiba yao imebana sana wanatoka asubuhi mapema na kurudi usiku saa mbili hivyo hawapati nafasi ya kusoma Mambo ya dini. Wanachofanya ni wakati wa likizo kuwaleta pamoja wanafunzi na kuwapatia mafunzo ya dini. Kwa upande wa Tabligh Tanzim inajitahidi kwenda sehemu ambazo hazijafikiwa ili kufikisha ujumbe wa Masih Aliyeahidiwa Hazrat Mirza Ghulam Ahmad (a.s)

Wajumbe kwa ujumla wao walimshukuru Huzur Anwar (atba) kwa kuwapatia semina hiyo na wakawa na matumaini kuwa semina za aina hiyo zitakuwa endelevu kwani zina faida kubwa katika kuongeza elimu.

Kwa siku hiyo ya kwanza semina ilifungwa saa kumi na mbili na nusu kwa maombi ya kimya kimya yaliyoongozwa na Amir na Mbashiri mkuu. Katibu wa Huzur alitoa wito kwa mjumbe yeyote anayetaka kumuona milango yake iko wazi na anaweza kufanya hivyo.

WASIYYAH

Kutoka Uk 11..

mpango huu, ili Mpango huu Mpya uweze kuja mapema kadiri iwezekanavyo, na siku zilizobarikiwa ziweze kudhihiri, na kila mahali bendera ya Islamu na Ahmadiyya ionekane ikipepea. Kwa wale
ambao tayari wameshafanya Wasiyyat wao natoa pongezi na kuwaombea. Na wale ambao bado, Mwenyezi Mungu awawezeshe kufanya hivyo, ili wao pia waweze kujikusanyia baraka za mali na za kiroho" Amin(Nizam Nau UK-132)

pia Hadhrat Khalifatul Masih V(atba) katika hotuba zake kadhaa ametukumbusha sehemu mbalimbali juu ya kuzingatia kujiunga na mpango huu wa Wasiyyat.
Huzur(atba) aliwahi kueleza kuwa,
"Kwa hiyo, tafuteni njia za kumpendeza Mungu, na katika enzi hii mojawapo ya njia hizi ni kujiunga na Mpango wa Wasiyyat kwa hivyo mnapaswa kuiendea haraka. Pia, Mpango wa Wasiyyat una mafungamano makubwa na Ukhalifa. Katika kitabu chake Al-Wasiyyat Masihi Aliyeahidiwa(a.s) aliandika kuhusu mambo mawili muhimu, mojawapo ya haya ni kudhihiri kwa kudra ya Pili baada ya yeye kufariki, yaani, kuanzishwa kwa Ukhalifa ambao ungedumu hadi siku ya kiyama. Maadamu kuna watu wanaoleta mabadiliko ya kiroho,basi kiwango cha taqwa cha Jumuiya kitaendelea kupanda, na kisha kupitia watu hawa wema wanaojitolea muhanga, Ukhalifa wa kweli wa Kiislamu wataendelea daima. kwa sababu Mwenyezi Mungu ameahidi Jumuiya ya watu wema Ukhalifa. Tunapaswa kuthamini zawadi hii na kushikamana nayo kwa ukamilifu, uaminifu na kujitolea. Kumbuka kwamba maendeleo yetu yote yanahusiana na Khilafat. Mwenyezi Mungu awajaalie nyote kuwa watiifu kwa Ukhalifa na kujiunga na Mpango wa Wasiyyat ili nyinyi na kizazi chenu muendelee kupokea baraka za Mwenyezi Mungu na muingie kwenye pepo ya radhi zake. Mungu awasaidie sana.
(Ujumbe wa Mwenzi kwa Ansullurah kuhusu Wasiyyat wa terehe 31/05/2005).
Pia Huzur(atba) akaendelea kutoa msisitizo zaidi,
"Katika hafla zilizotangulia vile vile nilielezea hamu yangu kwamba ... kati ya wanajumiyya wenye mapato na wanaolipa Chanda katika kila Jamaat, kunapaswa kuwe na angalau 50% ambao wamejiunga na mpango huu mkuu wa Masihi Aliyeahidiwa(a.s)"
(Gazeti la Afzal la 29-Jul hadi 11-aug-2005).
Hivyo katika ujumbe huu wa Huzur(atba) tunatakiwa kuuzingatia hasa wale walipaji wazuri wa Chanda Amma tukimbilie hima hima kujiunga na mpango huu wa Wasiyyat kwa kuitikia utiwo wa kiongozi wetu Mpendwa Khalifatul Masih V (atba) na mtu asisite kuiona idara ya wasiyyat kwa lengo la kuitikia wito huu wa Huzur. Mpaka sasa namba yetu wa wanachama wa Wasiyyat ina watu wapatao1000+ hivyo tunawajibu wa kuongeza idadi yetu ili tufikie lengo hili la Khalifatul Masih(atba).
Viongozi wa jamaat katika ngazi zote, aidha za Tanzeem au za Jamaat. Kuainzia ngazi za taifa hadi za matawi wote hawa Huzur ametukumbusha kufanya juhudi maalumu ya kujiunga na mpango huu wa Wasiyyat.
Huzur(atba) alisema kutumbusha viongozi kuwa,
"Jambo la kwanza ambalo ningependa kusisitiza ni kwamba viongozi wote wanapaswa kuwa sehemu yao
mpango wa Wasiyyat, kuanzia Majlis Amila ya kitaifa hadi ngazi ya chini kabisa. Hapo ndipo watakapoweza kuwausia wanachama wengine wa Jumuiya kuhusu wasiyyat".
(Alfazl la 31-Dec hadi 04-06 Jan 2005).
Wajibu wetu mkubwa kama idara ni kukumbusha na kuona kwamba tunafikia matarajio yaliyowekwa naKhalifa Mtukufu(atba) na kuifanya jamaat na Islam kuwa sehemu yetu ya kimbilio ili kupata radhi za Allah.
Waakhiri dawan anil-Ahmdulillah rabil alamini.

IMEANDALIWA NA IDARA YA WASIYYAT-TAIFA MAWASILIANO:
Katibu wa Wasiyyat: 0688 094211/0654 081914
Msaidizi Ofisi ya Wasiyyat: 0785 086527/0623 084840

Ukhalifa, Uongozi bora na uliotukuka

Na. Sheikh Karim-ddin Shamsi Sahib
Morogoro

خلافت کیا ہے ؟اک زندہ کرامت ہے محمد ﷺ کی
ہمیشہ رہنے والی اک نِظامت ہے محمد ﷺ کی

Ukhalifa kwa kweli ni muujiza hai wa Muhammad[saw]. na nidhamu ya kudumu milele.

Mwenye akili na busara kama **Bwana Hamayun Gohar** alisema akieleza umuhimu wa kupatikana kwa nidhamu ya Ukhalifa ndani ya Waislamu:

" Tunahitaji hewa safi itakayoweza kurekebisha umma, hilo litawezikana kuipitia idara ya Ukhalifa wa Waislamu."

Mtaalamu maarufu wa Misri Sheikh At-tan-tawi aliandika akieleza nafasi ya ukhalifa kwamba: "Yeyote anayetaka kuishi maisha ya amani ya kweli na ya furaha, yeyote anayependa maendeleo yake ya kiroho na ya kidunia, anatakiwa kutafuta bendera ya ukhalifa na kukaa chini yake. Awe na udugu hai na makao makuu yake na kupanga mipango yote ya maisha yake sambamba na mwongozo wake na yeyote atakayefanya hivyo atapata "-mafanikio ya kweli

(القرآن و العلوم العصرية ص ٢١.)

Ndugu wasomaji wa ***Mapenzi ya Mungu!*** Mwenyezi Mungu Alimumba binadamu kuwa kiumbe bora na kwa rasimu iliyo bora zaidi kati ya rasimu za uumbaji wake. na hii ndio kawaida yake Mungu Mwenye enzi iliyoenea katika Dunia hii kwamba huwatuma manabii kwa ajili ya kuwaongoza wanadamu wakati wa giza totoro na mbegu za uongozi wa kiungu unapandwa na Manabii kisha mbegu hii unaota na kukuwa. Kwa hakika, kuja kwa Manabi na mitume inakuwa dhihirisho la kudra ya kwanza ya Mwenyezi Mungu nao huitwa khalifa wa Allah Mtukufu Subahanahu wa Taalah. Manabi wameitwa ndani ya Kurani Tukufu kuwa Makhalifa Wake kama hadhrat Adam[as] na Hadhrat Dawud[as]. na bila shaka yoyote, cheo hiki ni cha kila nabii wa Allah Mtukufu. Kisha Allah. Ametoa ahadi kwa waaminio kwamba ukhalifa utapatikana kati yao kama ulipatikana kwa wale waliokuwa kabla yao katika aya 54 ya sura An-noor kisha anasema katika aya inayofuata kwamba:

وَاَقِيموالصلاةَ و اٰتوالزكوٰةَ و اَطِيعُوالرسولَ لعلكم تُرحمون.

Na simamisheni sala na toeni zaka na mtiini Mtume ili mpate kurehemiwa. Maneno haya ni dalili bayana juu ya jambo hili kwamba kuutii ukhalifa huu ni sawa sawa na kumtii Mtume ndio maana mara baada ya kupatikana kwa Ukhalifa tumeamrishwa kumtii Mtume ilahali Mtume ameshaondoka. Basi ukhalifa huu ni unaibu wa mtume na kuutii ukhalifa ndio kumtii mtume huyu saw. Kwa sababu hii tuna haki ya kusema kwamba: Ukhalifa wa Kiahmadiyya una umuhimmu mkubwa sana mno. Tunaweza kupata kujua daraja lake kwamba umeanzishwa na Mungu baada ya kufariki kwa nabii wake ili kukamilisha shabaha, lengona kusudio la kuja kwake na Allah ametoa ahadi ya kuusaidia daima dwamu na kutia baraka za kila namna kwenye shughuli zake hadi watu wanashangaa juu ya maendeleo na mafanikio yake hivyo anayepewa cheo cha ukhalifa anapata nuru ya unabii, fadhila, ubora na baraka zake. Cheo hiki kinapewa na Allah. khalifa hawezi kuondolewa kutoka cheo chake abadan asilan kwani anakuwa naibu wa nabii. Mungu anakuwa mwalimu wake na kumfundishia elimu na maarifa ya kina kabisa na kumja'alia waaminio wanaompenda na kuweka nafsini mwake mapenzi ya wafuasi wake.

Kama alivyosema Mtume Mtukufu saw kwamba:

خَيْرُ اَءِمَّتِكُم اللذين تحبونہم و ہم يحبونكم

Mabora wa maimamu wenu ni wale ambao mnawapenda nao pia wanakupendeni.

Imam uz zaman **Seyedna Ahmad**[as] alisema akieleza jambo hili kwamba: "Maana ya khalifa ni naibu ambaye hujadidisha dini. Wale watu wanaokuja kuliondoa giza linaloenea baada ya kuondoka kwa manabi, huitwa makhalifa." (Malfuzaat.j.4 uk.383).

Hazrat Mirza Nasir Ahmad, khalifa wa tatu wa seyyedna Ahmad a.s.alisema akifafanua Zaidi kwamba:

"Maana ya khalifa ni yule naibu wa mtume anayekuja wakati wa haja kwa ajili ya kujadidisha dini na kuzalisha ndani mwa(wafuasi) wao roho halisi ya dini na kuyatupilia mbali bidaa yote (mambo yaliozushwa ndani) ya Islam, na kuandaa mipango ambayo kwayo umma wa Waislamu waweze kupata rehema na Fadhili za Allah kwa wingi kadri wanavyoweza kuzipata." (Alfazal, Rabwah, 26 Decemba 1968)

Mwanzilishi Mtukufu wa Jumuiyya ya Waislam Waahmadiyya Hazrat Mirza Ghulam Ahmad[as] alisema akitubainishia **nafasi na daraja la ukhalifa** kwamba:

"Khalifa anakuwa naibu na naibu wa Mtume kwa maana ya uhakika ni yule tu ambaye anakuwa na sifa zilizokamilika (kama) za Mtume kuwa dhilli(mfano) yake, kwa sababu Mtume saw hakuwaita wafalme wadhalimu kuwa makhalifa kwani khalifa kwa kweli anakuwa mfano yaani dhill wa nabii, na kwa sababu mtu yeyote hawezi kubaki hapa duniani milele, hivyo Mwenyezi Mungu alipenda kwamba manabii ambao ni bora na wema zaidi kuliko watu wote wa dunia hii, wabaki duniani kwa njia ya mfano, Kwa hiyo Mwenyezi Mungu alipenda kuileta nidhamu ya ukhalifa ili watu wa dunia wasikose Baraka za utume muda wowote". (Shahadatul Kuran, R.KH.J.6.Uk.353)

Hadhrat seyyed Ismail shahiid r.a. aliandika:

"imam ni kama mwana mwenye bahati nzuri wa mtume na wakuu wote wa umma na watawa(watukufu) wote wa dini ni kama waajiriwa, wahudumu, watumishi na watumwa waaminifu (mbele yake)…kwa kifupi bila kumpitia yeye wazo la kupata ukaribu na Mungu ni wazo batili na wasiwasi za bure zisizokubaliwa na kukataliwa tu." (Mansabe Imamat,uk.78)

Anasema akiongeza kuwa:

Kushindana naye ni sawa sawa na kushindana na Kudra ya Mungu, na kumpinga yeye na kama kumpinga Mungu Mwenye Uwezo, kila ubora na sifa isiyotumika kwa ajili ya kumhudumia yeye ni fikra mbovu na kila elimu isiyotumika kwa ajili ya kubainisha adhma na shani yake ni bure tu. Kila mwenye sifa anayetaka kujilinganisha naye anashika njia ya kumshirikisha Mungu, hii ndio alama moja wapo ya wenye sifa kwamba wadumu katika kumhudumia yeye na kujishughilha katika kumtii yeye tu. [Mansab e Imamat uk.62-63]

Cheo au daraja la ukhalifa

Hazrat mirza Bashir Uddin Mahmood Ahmad khalifa wa pili anasema:

"Cheo hiki ni kikubwa kabisa baada ya unabii. Jamaa mmoja aliniambia kuwa tunajitahidi ili serekali akupe lakabu Fulani. Nimwambia lakabu hii itakuwa jambo la kwaida tu. Mimi naona cheo cha mfalme wa ulimwenguni pia ni duni kushindana na ukhalifa basi nawatoleni nasaha kwamba muwe na ucha-Mungu na adabu kwenye mambo yenu. Sipendi kamwe kwamba wapotee marafiki zetu wanaopata upinzani Fulani kwani kutokana na cheo cha ukhalifa wenye umri mkubwa pia ni kama Watoto kwangu na hakuna baba anyependa kuwa mwanae hata mmoja apotee."(Anwarul Uloom J.9.uk.425-426)

Kisha alisema akiekeza moja kwa moja daraja la Khalifa:

"Daraja la khalifa wa kiahmadiyya liko juu kuliko wafalme wote wa duni na viongozi wote. Yeye ni naibu au mwakilishi wa Allah na wa Mtume saw duniani."(Al-Fazal,27 Aug.1937 uk.8)

Khalifa wa pili wa Seyyedna Ahmad a.s. anasema:

"**Khalifa anakuwa cheo kikubwa zaidi kuliko Mujaddid** na kusimamisha sharia na kukimu dini ndio kazi yake hivyo Mujaddid angewezaje kuja wakati yeye(khalifa) yupo."

(Alfazal 8 April 1984)

Fadhila na ubora wa Khalifa: Hazrat Musleh Maud anasema:

"(mtu) ambaye Mungu anamwambia matakwa yake, ambaye Mungu anamshushia funuo zake, ambaye Mungu amemteua kuwa imam na khalifa wa Jamaati, mnaweza kuzitekeleza shuguli zenu kwa kushauriana naye na kwa mwongozo wake. Shughuli zenu zitabarikiwa jinsi mtakavyojiunganisha naye na shuguli zenu zitakosa baraka kadri mtakavyokaa mbali naye. Kama tawi lile tu linaweza kuzaa matunda ambalo limejiunganisha na mti na tawi lile lililokatwa na kutupwa mbali na mti haliwezi kuzaa matunda, hali kadhalika mtu yule tu anaweza kuifanyia kazi silsila hii anayejiunganishia na imamu. Kama mtu yeyote hajiunganishii na imamu ingawaje anazijua elimu zote za dunia, hawezi kufanya kazi hata kama anavyoweza kufanya ndama wa mbuzi.

(Al-Fazal, Qadian.20 nov.1946)

Khalifa wa pili wa Hazrat Ahmad A.S. anasema:

"Maana ya ukhalifa ni haya tu kuwa neno lolote linapotoka kutoka midomo ya khalifa basi tuyaache kabisa mipango yote, mapendekezo yote, na rai yote wakati ule ule, kisha tuelewe kwamba sasa utafaa mpango ule ule, pendekezo lile lile na rai ile ile iliyotolewa na khalifa, bila ya kujifunza roho h hii, hotuba zote ni bure, mipango yote ni batili na hila zote hazitafaa. (hotuba ya Ijumaa ya 24 January 1936)

Nabii anahaki juu ya waaminio

اَلنَّبِيُّ اَوْلىٰ بِالمُومِنِينَ مِنْ اَنْفُسِهِمْ و اَزْوَاجُہ اُمَّهَاتُهُمْ.الاحزاب.٧.

Nabii ni muhimu kwa waaminio kuliko nafsi zao na wake zao ni mama zao.

Kuna ukoo maarufu wa jimbo la Punjab unaoitwa noon family na bw. Fairooz khan Noon alwahi kuwa Waziri mkuu wa Punjab katika utawala wa Uengereza na kaka yake bw. Malik noon khan alikuwa muahmadiyya naye alikasirika kwa mdogo wake fairooz khan katika baadhi ya mambo ya urithi lakini kutokana na heshima kubwa ya kaka mdogo wake alishindwa kuongea naye na kuomba radhi kwake hivyo basi alitafuta njia ya kumridhisha kaka na kupeleka ujumbe wa khalifa wa pili ndipo khalifa alimuita na kumwambia kwamba

Ukurasa wa 10

Bustani ya Washairi

HAE MSIBA MZITO!

Simu inaita.
Mara inapokelewa.
Assalaam Alaikum Amir Sudi.
Anajibu, Sauti ya Kiza.
Namwambia; Innaa lillaahi wa inna ilaihi raajiuun. Tunao msiba mkubwa.
Kabla sijamaliza, anatoa ubeti wa Shaabani Robert;
Siku ya mauti kuja mtu hana kimbilio,
Kuja budi itakuja, kama si kesho ni leo,
Kila mtu humfuja, pasi ya mapendeleo,
Habaki mtu mmoja katika safari hiyo.
Nami kabla sijampa habari hiyo nzito, namkumbusha ubeti wa Sheikh Kaluta Amri Abedi kwa Mahmood Hamduni (Jjitu kali).

Pole bini Hamduni kufa pia ni rehema,
Tungedumu duniani pasi kufa na kuhama,
Tungekuwa mashakani kwani dunai si njema,
Huna baba huna mama uwe na Mola Rahima.

Ananiuliza; Nipe habari nani katangulia?
Namjibu; Alhaji Ali Hassani Mwinyi.
Anajibu; Innaa lillaahi wa inna ilaihi raajiuun. Ni msiba mzito kwetu.
Unajua Mahmood; Mimi nilifahamiana sana na Alhaji Alli Hassani Mwinyi, wakati naandika kitabu juu ya ushairi, mara kwa mara nilikuwa nikienda kwake ili kubadilishana mawazo. Na kila nilipokwenda alinipokea kwa bashasha. Bwana huyu alikuwa muungwana. Mpokeaji mzuri wa wageni. Kwa kiswahili simuoni kama yeye. Kwa msamiati na ufasaha wa matamshi ananikumbusha Sheikh Muhammad Alli (Al-Bukhri) na Sheikh Abdul Bari Diwani.

Namwambia; Nakuomba bw. Amir ututungie shairi zuri la kuomboleza.
Anajibu; Umenipa kazi kubwa. Siku hizi situngi. Lakini kwa sababu ombi limetoka kwako kwa niaba ya Mapenzi ya Mungu, Insha Allah kazi hiyo nitaifanya.

Baada ya siku tatu napata simu, nakwenda kwake nakuta shairi lifuatalo tayari;

HAE MSIBA MZITO!
Kwa jina la Rahmani, Rahimu mwenye nemsi
Wa mbingu na ardhini, wa ajinani na insi
Ndu yetu Alli Hassani, ewe ilahi Kudusi,
Umfanyie wepesi, leo na siku adhimu.

Leo na siku adhimu, umfanyie wepesi,
Umpe yalo matamu, kwenye yako Majlisi,
Kwenye Jannati naimu, yawe makazi halisi,
Kwako twakuomba sisi, ume Ali Hassani.

Awe mbali na balaa, za shetani ibilisi
Pia mbali na nadhaa, na moto na wasiwasi
Peponi ende kukaa, salama firidausi,
Tukubalie Mkwasi, Mkubalifu duaa.

Na wakezi na watoto, waepushe na mikosi,
Uwaruzuku mapato, ya halali kwa nafasi,
Katu wasende kushoto, dunia isiwaghasi,
Wafanye ya ufanisi, ya Ali Hassani Mwinyi.

Ubeti huu shairi, hapa nimesema basi,
Nasema basi Amiri, sitafikia sudisi,
Ayakubali Kahari, yale niliyoandisi,
Amina Rabbi Mkwasi, kwa Ali Hassani Mwinyi.

WAKATIKA TUNAKWENDA MITAMBONI TUMEPOKEA TAARIFA YA MSIBA WA KUONDOKEWA NA MSHAIRI MAARUFU WA KISWAHILI AMIR SUDI ANDANENGA - SAUTI YA KIZA, ALIYEFARIKI MEI MOSI 01/05/2024. HABARI ZAIDI KATIKA TOLEO LIJALO INSHAALLAH

Tumia nafasi uko

Furusa zinazokuja, hazitobaki daima
Zifungie mkoja, huwo ndo wakati mwema
Sikuhadae vileja, ukashindwa tenda mema
Tumia nafasi uko, ikitoka imetoka

Shuleni unapokuwa, soma vile unaweza
Ajira unapopewa, jitume bila buruza
Jukumu ukipangiwa, usahihi tekeleza
Tumia nafasi uko, ikitoka imetoka

Pesa unapoishika, sisahau kuigawa
Wazazi pate baraka, familia kutumiwa
Usiache na sadaka, Kuwekeza nakukuwa
Tumia nafasi uko, ikitoka imetoka

Dunia yetu hadaa, haiachi kupumbaza
Leo utaishangaa, kesho itakuponza
Na dhambi zinazagaa, Dunia Iko ajuza
Tumia nafasi uko, ikitoka imetoka

Wema hauna wakati, sio kesho nitafanya
Mimi nikijana eti, kizeeka nitafanya
Hujui Yako bahati, mauti itakufinya
Tumia nafasi uko, ikitoka imetoka

Masihi omary stambuli kisagwa

KULISHA

Halishwi yeye hulisha, Rabbi mtoa riziki
Sifa hino inatisha, nani anaimiliki?
Nani aweza kuvisha, lau lapa la kaniki?
Udongo walima pamba, nani kautengeneza?

Mahmood Hamsin Mubiru –(Wamamba)
Kiwalani - Dar es salaam.

SALA NI KUMBUKO BORA

Assalam alekum, mahdi lompokea
Ninaujumbe adhiim, kaa chonjo kusikia
Sala ni nguzo muhim, Allah kumkaribia
Sala ni KUMBUKO bora, kwa muumba wa dunia.

Baada ya ashahadu, sala tano zafwatia
Wahid kumuabudu, kwa jazba na kulia
Msaada kwa samadu, kwake ukitegemea
Sala ni KUMBUKO bora, kwa muumba wa dunia.

Kwa sala tamkumbuka, muumba wetu jalia
Quran tatamka, na sifa kimtolea
Machozi yatakutoka, maombi kinyenyekea
Sala ni kumbuko bora, kwa muumba wa dunia.

Kisimama tamtaja, sifa za kuhimidia
Utaukiri umoja, pekee msujudia
Mtume utamtaja, durud kimsalia
Sala ni kumbuko bora, kwa muumba wa dunia.

Kwa haya naweka loma, japo mengi menijaa
Kumkumbuka karima, ni kwa sala kupitia,
Manane ukasimama, sifa zake kisifia
Sala ni kumbuko bora, kwa muumba wa dunia

SIKU YA IDILFITIRI NI SIKU YENYE BARAKA.

Bismillah naanza,rahman rehemeza,
Allah ndiye wa kwanza,na vingine twafatiza,
Hapa ndio naanza,beti kuzipangiliza,
SIKU YA IDILFITIRI NI SIKU YENYE BARAKA.

Yarabi mola Azizi,nakuomba niauni,
Yote yawe na mizizi,ntayo weka utungoni,
Yasiwe ya kipuuzi,nikawamo hasarani,
SIKU YA IDILFITIRI, NI SIKU YENYE BARAKA.

Leo hii kwa yakini,sote tunafurahia,
Twamshukuru manani,siku hii kufikia,
Kumaliza Ramadhani,sote tunashukuria,
SIKU YA IDILFITIRI,NI SIKU YENYE BARAKA.

Twatakiwa kuombea, kuomba kwake Manani,
Na fitiri kuzitoa,sio kujificha ndani,
Ili awezepokea,saumu za Ramadhani,
SIKU YA IDILFITIRI,NI SIKU YENYE BARAKA.

Mola keshatuambia,ndani ya Qur'ani,
Ni lazima kufungia,saumu za Ramadhani,
Ili tuweze fikia,tupate uchamunguni,
SIKU YA IDILFITIRI,NI SIKU YENYE BARAKA.

Leo twasherehekea,siku iliyo adhimu,
Ndugu zangu nawambia,tusilevywe na vitamu,
Sala tukazikimbia,nazo ndizo za muhimu,
SIKU YA IDILFITIRI,NI SIKU YENYE BARAKA.

Tule tunywe na kusaza,mola livyo turuzuku,
Allah tumweke wakwanza,tumwabudu kila siku,
Yale alo tukataza,tuyapige marufuku,
SIKU YA IDILFITIRI,NI SIKU YENYE BARAKA.

Ibada tuendeleze,kwa myezi inofuata,
Tahajudi tusibeze,tukabaki jikunyata,
Kutoa tusikwepeze,kwa kila tutacho pata,
SIKU YA IDILFITIRI,NI SIKU YENYE BARAKA.

Nyote idimubaraka,mliomo humu ndani,
Mola atie fanaka,humo mwenu mioyoni,
Pia atie baraka, huko kwenu majumbani,
SIKU YA IDILFITIRI,NI SIKU YENYE BARAKA.

Tamati nafunga kazi, kalamu naweka chini,
Namwomba mola azizi,atwepushe na shetani,
Tusije kupiga mbizi,tuingie hasarani,
SIKU YA IDILFITIRI,NI SIKU YENYE BARAKA.

Sharifu.A.Nyamihas.
Kagenyi, Kyerwa, Kagera.

KUYAKUMBUKA SIWEZI
Muhali kuyakumbuka, makosa niliyotenda
Ila umeyaandIka, ya kheri na yenye inda
Ninakuomba Rabuka, nyoosha palipo pinda.
Wewe Shadidul iqabu, ila pia husamehe

Mahmood Hamsin Mubiru –(Wamamba)
Kiwalani - Dar es salaam.

Hadithi ya Kutia Moyo: Wewe ni wa thamani sana kwa wale wanaokupenda

Farasi na Mbuzi

Kulikuwa na mkulima ambaye alikuwa na Farasi na Mbuzi. Siku moja, Farasi aliugua na mkulima akamwita Daktari wa Mifugo, ambaye alisema: Kweli, Farasi wako ana virusi. Lazima anywe



dawa hii kwa siku tatu. Nitarudi siku ya 3 na ikiwa hayuko bora, lazima tumzike. Jirani, Mbuzi alisikiliza kwa makini mazungumzo yao.

Siku iliyofuata, walimpa dawa na kuondoka. Mbuzi akamsogelea Farasi na kusema: Uwe hodari, rafiki yangu. Inuka la sivyo watakuzika!

Siku ya pili, wakampa dawa na kuondoka. Mbuzi akarudi na kusema: Njoo rafiki, inuka la sivyo utakufa! Njoo, nitakusaidia kuamka. Twende! Moja mbili tatu!

Siku ya tatu walikuja kumpa dawa na Daktari wa Mifugo akasema: Bahati mbaya itabidi tumzike kesho. Vinginevyo, virusi vinaweza kuenea na kuwaambukiza Farasi wengine. Baada ya wao kuondoka, Mbuzi alimwendea Farasi na kusema: Sikiliza rafiki, ni sasa au kamwe! Inuka, njoo! Kuwa na ujasiri! Haya! Simama! Hiyo ndiyo, polepole! Kubwa! Njoo, moja, mbili, tatu! vizuri. Sasa haraka, njoo, Ajabu! Kukimbia, kukimbia zaidi! Ndiyo! Ulifanya hivyo, wewe ni bingwa!

Farasi aliinuka kwa bidii kubwa. Baada ya kutiwa moyo zaidi kutoka kwa Mbuzi, alitembea kwa miguu kisha akaruka.

Ghafla, mkulima alirudi, akamwona Farasi akikimbia shambani na akaanza kupiga kelele: Ni muujiza! Farasi wangu amepona. Lazima tuwe na sherehe kubwa. Tuchinje Mbuzi!

Maadili ya hadithi: Hii mara nyingi hufanyika mahali pa kazi. Hakuna anayejua kwa hakika ni mfanyakazi gani anastahili sifa ya mafanikio, au ni nani hasa anayechangia usaidizi unaohitajika ili kufanya mambo yafanyike.

Kumbuka: Kujifunza kuishi bila kutambuliwa ni ujuzi! Kwa hivyo, ikiwa mtu yeyote atawahi kukuambia kuwa kazi yako si ya kitaalamu, basi kumbuka: Wastaafu walijenga Safina [ambayo iliokoa viumbe vyote] na wataalamu walijenga Titanic [wote walikufa kwa huzuni].

JIFUNZE KUISOMA NA KUIELEWA BIBLIA TAKATIFU NA QUR-ANI TUKUFU:- 28:50--51:

...Kutoka toleo lililopita

NYOKA NI MTU, watu au Jamii yenye tabia mbaya tena ni waongo na Wanafiki, Mt 23:33--34; M-MBWA MWITU NI Mtu au watu wanafiki na wanaoupinga ukweli Kwa ukari Mt 7:15; M-MBWA NI Makabira mengine yasiyo ya Wana wa Israel. Mt 15:26; NGURUWE NI makabira mengine yasiyo ya Wana wa Israel. pia Mtu au watu wanaoyadharau na kuyaharibu maneno ya mungu Mt 7:6; KIPOFU, KIZIWI, BUBU, KIWETE, NK. NI-- Watu wasiotaka kufuata MFUMO WA MUNGU na wanaopuuza mafundisho ya Mwenyezi Mungu Mt 13:13--15;

SHETANI NI Mtu, Watu au jamii yenye tabia mbaya Wasio yawaza ya mungu. Mt 16:23; Yoh 6:70--71; IBILISI NI Mtu, watu au Jamii yenye tabia mbaya.
Yoh 8:44; MAUTI AU KIFO NI Kutengana kiwiliwili na Uhai wa KIMWILI au kiimani (kiroho) na Pia ni matatizo makali yanayokaribia KIFO. Mt 8:21--22; na 1wakor 15:30--31; Je aliyekufa KIMWILI anaweza kumzika mwenzie !!?? Je Kuna MTU anaekufa kilasiku, !!??

MILELE NI Muda mlefu uliokadiliwa na Mwenyezi Mungu. UKOMO upo, Daniel 5:10, 6:21;Wako wapi wafalme hao.
ULIMWENGU NI Himaya KUBWA ya utawala, Luk 2:1--4; mdo 24:5; Est 8:9--11; NENO NI-- Mpango au wazo, Yoh 1:14 na 1:30--34; Mt 21:33--44; Waifeso 4:29; Yohana 1:30-34

Huyu ndiye niliyenena habari zake ya kwamba, Yuaja mtu nyuma yangu, ambaye amekuwa mbele yangu; kwa maana alikuwa kabla yangu. Wala mimi sikumjua; lakini kusudi adhihirishwe kwa Israeli ndiyo maana mimi nalikuja nikibatiza kwa maji. Tena Yohana akashuhudia akisema, Nimemwona Roho akishuka kama hua kutoka mbinguni; naye akakaa juu yake.

Wala mimi sikumjua; lakini yeye aliyenipeleka kubatiza kwa maji, huyo aliniambia, Yeye ambaye utamwona roho akishuka na kukaa juu yake, huyo ndiye abatizaye kwa Roho Mtakatifu.
Nami nimeona, tena nimeshuhudia ya kuwa huyu ni Mwana wa Mungu. Mpango huo Mwenyezi Mungu alimjulisha YOHANA pia,

NDANI YA MUNGU NI-- Kushikamana na maagizo ya Mwenyezi Mungu. Yoh 17:21--23; 14:20--25; 15:7--10; 20:17; Waifeso 4:6; Tafadhali nduguyangu msomaji dhamira yetu ni kukutoa katika Giza kukupeleka kwenye mwanga wa kweli Ili umtukuze mungu wa kweli. Faidika na Nuru hiyo angalau Kwa uchache tu.
Maandiko ya muundo huo Yako mengi sana kwenye Vitabu vya Dini tafadhali fuatilia somo hili. No 2 ni Qur-ani tukufu.
Neno letu la mwisho ni UPENDO KWA WOTE BILA YA CHUKI KWA YEYOTE

JINSI YA KUPIKA UBUYU WA ZANZIBAR

Mahitaji ya Ubuyu wa Zanzibar

1.Sukari vikombe 2, Maji vikombe 2, Nusu kikombe unga wa ubuyu, Vikombe 4 ubuyu wenyewe, 1/4 pili pili ya unga, 1/4 tsp chumvi, 1/4 tsp iliki ya unga, Rangi nyekundu au yeyote ile utakavyopenda na Vanilla(kama utapenda).



MATAYARISHO YA UBUYU WA ZANZIBAR

1.Katika sufuria,weka maji na sukari na chumvi na pili pili ya unga na Rangi na iliki. Moto uwe juu kiasi na changanya vyote hivyo vipike vizuri.

2.Wakati vitu vinaanza kujipika utakuta rojo linatoa mapovu. Endelea tu kukoroga acha rojo lipikike vizuri. Baada ya hapo mapovu yakianza kutulia inamaanisha kua rojo limeanza kua zito.

3. Sasa hapo chota kidogo katika mwiko na test kwa vidole kama rojo linanata ua halinati. Rojo linatakiwa linate ndio linakua limeiva. Lisinate Sana kiasi tu.

4. Baada ya mchanganyiko wako kuiva ipua hayo maji sasa Chukua beseni au sufuria chini weka ubuyu wako ndani ya beseni Anza kumimina hiyo juice yako kidogo kidogo huku ukiuchanganya kwa mikono safi.Ila hakikisha pembeni una Unga wa ubuyu ulio changanywa na mchanganyiko huo huo.

5. Baada ya ubuyu wako kuchanganyika vizuri (usiwe rojo) Anza kumiminia ule unga kwa juu ili uwe mkavu mkavu na kutoa ule ubichi alafu uanike ukishapoa ubuyu tayari kuliwa.

NOTE:UNGA WA UBUYU MKAVU LAZIMA UCHANGANYIE NAO PIA PILI PILI,ILIKI NA RANGI

ANGALIZO:Hatua ya 4 ni muhimu sana hakikisha mchanganyiko unamimina kwenye ubuyu mkavu na sio kuchukua ubuyu mkavu na kuupikia.Tunafanya hivyo ilikufanya ubuyu uwe mlaini na usiwe mgumu wakati wakula.

USIPO ZINGATIA STEPS NILIZO KUPA BASI JIANDAE KUTOA UBUYU ROJO KILA UKIANDAA.

TANGAZO

Tanziim ya Lajna Imaillah Tanzania

Taanzim ya lajna imaillah Tanzania inapenda kuwatangazia Lajna na Nasrat wote nchini kuwa Ijtmaa ya Lajna na Nasrat 2024 inatarajiwa kufanyika katika eneo la Jamaat Kitonga Dar es salaam tarehe 28 na 29 Juni 2024 ikifuatiwa na Shura siku ya Jumapili tarehe 30 Juni 2024 InshaAllah .

Hivyo Lajna na Nasrat wote wanakumbushwa kufanya maandalizi kwa ajili ya Ijtmaa yetu kama barua ya Ijtimaa inavyoelekeza. Pia wanakumbushwa kuchangia mchango wa Ijtimaa kiasi cha Shilingi 12,000/= kwa Lajna na 3,600/= kwa Nasrat. Allah atujaalie wote tuweze kushiriki ili kufanikisha Ijtmaa yetu InshaAllah

Sadr Lajna Taifa
Zena Nyange.

Jamia Ahmadiyya Waadhimisha Siku ya Masihi Aliyehidiwa[as] kwa Kugawa Zawadi ya Vyakula



Tarehe 23 Machi kila mwaka waislamu wa Ahmadiyya kote ulimwenguni hufanya maadhimisho ya kihistoria kukumbuka siku ambayo mjumbe wa Mwenyezi Mungu katika zama hizi za mwisho Hazrat Mirza Ghulam Ahmad[as] wa Qadian alipoanza kuchukua bai'at kwa mara ya kwanza kwa amri ya Mwenyezi Mungu Mtukufu katika mwaka 1889.

Hapa nchini mikoa na matawi mbalimbali pia hufanya maadhimisho ya siku hii kwa kufanya mikutano na kuwaalika wageni mbalimbali.

Jamia Ahmadiyya nayo ipo mstari wa mbele katika kuadhimisha siku hii adhwiim kila mwaka, katika mwaka huu wa 2024 maadhimisho ya siku ya masihi aliyeahidiwa a.s yalifanyika siku ya jumamosi ya tarehe 23/03/2024 kuanzia saa 4:30 asubuhi mpaka saa 6:30 mchana. Maadhimisho haya yalifanywa katika ukumbi wa chuo chetu cha Jamia Ahmadiyya uliopo katika eneo la chuo kilichopo kihonda katika Manispaa ya Morogoro Mjini. Mgeni rasmi katika maadhimisho haya alikuwa ni mkuu wa Wilaya ya Morogoro Mheshimiwa Bi Rebeca Msemwa, pamoja naye walikuwepo pia diwani wa kata ya kihonda maghorofani mheshimiwa Hamisi Ndwatta wenye viti wa mitaa yote 9 ya kata ya kihonda pamoja na viongozi wa Chama cha Mpinduzi kata ya kihonda Maghorofani. Aidha maulana Sheikh Mahmood Chaudry Sahib Amir na mbashiri mkuu hapa nchini alikuwa ni mgeni maalumu.

Mwenyekiti wa hafla alikuwa ni Maulana Sheikh Abid Mahmood Bhatti Sahib mkuu wa chuo cha Jamia Ahmadiyya na Naibu amir wa Jamaat. Hafla ilianza kwa usomaji wa Qur'an tukufu iliyosomwa na Hafidh Abdulrahman R. Rundo na kufuatiwa na shairi la Kiswahili lililosomwa na Abusswiddiq A. Pembe, kisha mwenyekiti wa hafla alifanya utambulisho maalumu wa wageni waalikwa.

Baada ya utambulisho huo mfupi, ilifuata hotuba maalumu ya hafla iliyokuwa na maudhui isemayo "Mafundisho ya Hazrat Masihi Mau'ud[as]", hotuba hiyo iliyotolewa na sheikh wetu wa mkoa wa morogoro Maulana sheikh Karimuddin Shams sahib, katika hotuba yake sheikh sahib alianza kwa kunukuu aya ya 30 kutoka katika suratul fat'h (48:30), kisha akagusia itikadi za dini kuu tatu za Uyahudi,Ukristo na Uislamu juu ya uhai wa Hzrat Masihi Issa[as] mbinguni na kisha akanukuu mafundisho ya Hazrat Masihi Mau'ud[as]

akithibitisha itikadi hiyo mbovu na kisha kueleza mafundisho sahihi juu ya suala hilo na muradi wa kurudi kwa Hazrat Masihi Bin Mariamu[as]. Sheikh Sahib alieleza kwa urefu mafundisho sahihi ya Hazrat Masihi ma'ud a.s juu ya kuwatendea wema watu wote na kuwahurumia pia viumbe wote wa Allah. Sheikh Sahib alinukuu matukio kadhaa katika maisha ya Masihi aliyeahidiwa[as] kuthibitisha na kukazia hotuba yake ambayo iliwavutia sana wasikilizaji.

Baada ya hotuba hiyo ya sheikh wa mkoa wa morogoro, zilifuata nasaha chache kutoka kwa diwani wa kata ya kihonda Maghorofani Mheshimiwa Hamisi Ndwatta, ambaye katika maelezo yake alishukuru sana (jamaat) kwa ushirikiano mzuri inayotoa, hususani katika shughuli za kimaendeleo katika jamii, akitaja baadhi yake kama vile kuchangia ujenzi wa shule zilizomo katika kata hii, zahanati ya kata, kazi za kujitolea (waqar e amal) zinazofanywa katika majengo ya uma nk. Baada ya hapo ilifuata hotuba fupi ya mgeni rasmi ambaye katika hotuba yake alianza kwa kuishukuru sana Jamaat kwa kuwakumbuka wahitaji katika jamii na ushirikiano mzuri na ukaribu na viongozi wa serikali kuanzia ngazi za mitaa hadi mikoa na Taifa kwa ujumla, aidha aliipongeza sana jamaat kwa mchango mkubwa katika malezi ya vijana kwa kuanzia shule kwa ajili ya elimu dunia na jamia kwa ajili ya elimu ya akhera, pia aliipongeza jumuiya kwa kuadhimisha siku hii kwa

Ukurasa 09

MATUKIO KATIKA PICHA

Jamia Ahmadiyya Waadhimisha siku ya Masihi aliyehidiwa[as] kwa kugawa Zawadi ya vyakula





kuwakumbuka wasiojiweza kwa kuwagawia zawadi ya chakula, alisema kwa hilo ni jambo lenye kumpendeza sana Mwenyezi Mungu na kuwaasa wanajumuiya kuendeleza utamaduni huo.Pia mheshimiwa mkuu wa wilaya aliahidi kutoa ushirikiano wa karibu na jamaat muda wowote atakapohitajika.

Baada ya hotuba hiyo ya mgeni rasmi, ilifuata hotuba ya Maulana Sheikh Tahir Mahmood Chaudry sahib. Amir sahib alianza hotuba yake kwa kunukuu Al'imraan (3:93) ambamo Allah anasema "***Hamtaweza kuufikia wema hasa mpaka mtoe katika vile mnavyovipenda…..***" kisha Amir sahib alieleza falsafa ya kujitolea katika njia ya Mwenyezi Mungu na kuongeza kuwa kujitolea kuwe ni kwa ajili ya kupata radhi ya Mwenyezi Mungu na si vinginevyo. Kisha Amir sahib alisoma aya za 9-10 kutoka katika ***Suratu Ddahar*** (76:9-10) ambazo tafsiri yake ni kama hivi "Na huwalisha chakula masikini na yatima na mfungwa kwa mapenzi yake Allah. (Husema): Tunawalisheni kwa ajili ya radhi ya Mwenyezi Mungu tu, hatutaki kutoka kwenu malipo wala shukrani". Kisha Amir Sahib alinukuu kauli mbalimbali kutoka katika maandiko ya Hazrat Masihil-Mau'ud[as] zinazosisitiza juu ya kuwapenda na kuwahudumia watu wote bila ya kujali tofauti za imani,rangi,kabila nk. Na akaongeza kusema kuwa daima jamaat Ahmadiyya inajali na kuthamini utu wa mwanadamu, amani na utulivu katika jamii na kaulimbiu yetu isemayo ***"Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote",*** ni ushahidi wa hili. Kisha Amir Sahib alieleza maana sahihi na ya kweli ya neno "jihad"yakuwa neno hili maana yake ni mtu kupambana na matamanio mabaya ya nafsi na amma kuchukua silaha na kuua watu, haya sio mafundisho ya Islamu.

Mwisho Amir Sahib alimshukuru mgeni rasmi (mkuu wa wilaya) kwa kukubali mwaliko wetu licha yakuwa na majukumu mengi, kisha Amir Sahib aliongoza maombi ya kimya na kupiisha zoezi la ugawaji wa zawadi, ambapo mwaka huu wahitaji wa mitaa yote 9 ya kata ya kihonda maghorofani wamefikiwa na kufaidika na zawadi hizo zaidi ya kaya 160, zawadi zilizotolewa ni Unga na Mchele.

Ukhalifa, Uongozi bora na uliotukuka

Kutoka Uk.05

asuluhishe mambo yake hata kama analazimika kuacha haki zake basi Bw. Malik Khan Noon alienda mwenyewe kwa mdogo wake na kumwambia kuwa yeye yuko tayari kwa maamuzi yoyote atakayoufanya. Baadaye mambo yaliposuluhika Huzur alimwambia bw.Malik khan Noon kwamba: mimi nilikuomba wewe kwani **ninahaki juu yako na juu ya mali yako** kwani wewe ni mfuasi wangu na tangu siku ile ninakuombea dua kila siku.

Kuna Sheikh fulani,ameweka clip moja ya video kwenye **youtube** ambamo, Hazrat Chauhdary Zafrullah Khan, Dr. Abdus Salam na Mirza Muzaffar Ahmad sahib wapo wamesimama mbele ya khalifa mtukufu wakiinama vichwa vyao. Sheikh yule ameandika juu ya picha hiyo kwamba hao wote watatu ni mabwana wenye madaraka ya ulimwenguni lakini wamesimama mbele ya Khalifa wao kama Watoto wa darasa la kwanza kisha yule sheikh anasema kama yeyote kati yetu yaani wa dhehebu lake, anapoweza kujisomea kiasi tu basi anaanza kujielewa kuwa mtu mkubwa na kuacha kabisa kuonana nasi.

Tungependa kumuelezea sheikh huyu na wenzake wote kwamba, wanajamaati wanafahamu vyema cheo na daraja la ukhalifa na kufuata maamrisho yake, na kuelewa vyema adabu na taratibu zote za heshima kwa ajili ya khalifa wetu mpendwa. Wanahistoria wa Islam wameandika matukio kadhaa ya kumheshimu na kumtii khalifa wa zama na ndani ya Jumuiyya pia yameripotiwa matukio ya aina yake kwa mfano Mian Abdullah Sanori r.a.,mir Mahdi Hasan walivunja sala zao kwa kusikia sauti ya imam wao kisha Hazrat Maulana Noor ud din r.a.pia alipoitwa na Hazrat Masihe Maud A.S. alikuwa anasali na aliposikia tu sauti yake mara alivunja sala na kufika kwa Huzur. Baadhi ya watu walipouliza juu ya hilo basi Hazrat Masihe Maud[as] alisoma aya hii ya Kurani akiwajibu kwamba:

لا تجعلوا دعاالرسول بينكم كدعاءِبعضكم بعضا (النور:64) Msifanye kumuita Mtume baina yenu kama mnavyoitana nyinyi kwa nyinyi.

Hazrat Musleh maud r.a. alisema: "ni juu yenu kwamba kila mnaposikia sauti ya mjumbe wa Allah basi muitikie mara moja na kukimbia kabisa ili kuitimiza kwani siri ya maendeleo yenu imefichika humo bali kama wakati ule mtu anakuwa anasali hata hivyo ni jukumu la kwake kumsikia Mtume wa Allah akivunja sala yake na amri hii inamhusu khalifa wa Mtume wa Allah pia.na ni lazima kujumuika kwa sauti yake na kutoroka kutoka kikao chake(khalifa) pia ni dhambi kubwa mno"(Tafsire Kabir j.6.uk.409)

Tunaelewa vizuri kuwa: kuikuza, kuhishimu na kuitii nidhamu iliyoanzishwa na khalifa wa zama ni sawa sawa na kuhishimu khalifa wa Mungu.

Ndugu zangu wapendwa! Naibu wa mtume kwa kuwa anashika nafasi yake basi anastahiki heshima, adabu na itifaki zile zile zinayotolewa kwa ajili ya nabii. Mwenyezi Mungu Ameeleza siri hii kwenye aya kadhaa za Kurani Tukfu kwa mfano amesema:

مَنْ يُّطِعِ الرَّسولَ فَقَدَاَطَاعَ اللّٰہَ۔ النساء:۸۱۔

Anyemtii mtume bila shaka anamtii Allah.

Na bwana wetu Mtume[saw] alisema akibainisha Zaidi kwamba: anayenitii mimi anamtii Allah, na anayeniasi mimi, anamuasi Allah na anayemtii Amiri ananitii mimi na anayemuasi amiri basi ananiasi mimi. (Sahihul Bukhari,kitabul Jihad)

Hivyo kumtii khalifa wa mtume ni kumtii mtume na kumuasi khalifa ni sawa sawa na kumuasi mtume.

Seyyedna Ahmad a.s. anasema,

"Maana ya khalifa ni naibu anayejadidisha dini. Wale (watu) wanaokuja kushika nafasi za manabii baada yao kwa ajili ya kuliondoa giza linaloenea baada ya zama za manabi huitwa Makha lifa."(Malfoozat,J.4.UK.383)

Kuwa naibu wa nabii khalifa anashika daraja la juu kabisa katika kujadidisha dini kuliko watukufu wengine wote wanaoitwa Mjaddid au Mawalii n.k.

Sawa na hadithi ya bwana wetu Mtukufu Mtume Muhammad[saw]. ukhalifa utapatikana tena kwa njia ya unabii baada ya Masihi Aliyeahidiwa na Masihi Aliyeahidiwa a.s. ameshabainisha kinaga ubaga kuwa ukhalifa wake utadumu milele hadi siku ya Qyama hivyo basi Mwenyezi Mungu Ameshapanga kuwa Islam itaendelea kujadidishwa na kuhuishwa kwa ukhalifa wa Hazrat Masihe Maud[as]. mpaka siku ya Qyama na silisila hii itaendelea ndani ya Jamaati yake tu.

Hadhrat Ally ra. Khalifa wa 4 wa Mtume[saw] alisema akitoa bishara kwamba: atakapo kuja Imam Mahdi basi Allah Mtukufu Atawakusanya watu wa mashariki na wa magharibi kwa ajili yake. (**ينابيع المودة جلد ٣ ص ٩٠)**

Mu'ujiza huu tunashuhudia kila siku kutokana na baraka za ukhalifa kwamba watu wa mashariki na wamagharibi, watu wa kusini na wa kaskazini wanaendelea kujumuika chini ya bendera ya ukhalifa wa Kiahmadiyya na maelfu ya watu wanachukua Bai'ati ya Imamu wa zama kutika kila kona ya dunia.

Bwana Saqib Zerwi mtumishi maaruf wa Silsila aliweza kuitumikia dini kwa muda mrefu oficini kwake khalifa lakin alikuwa na utaaluma kama mwana Habari na aliwahi kuwa mhariri mkuu wa jarida la Lahore na kufungiliwa kesi nyingi dhidi yake kwa sababu alikuwa anachapisha sana Habari za Jamaati. Yeye anasema siku moja mimi na Rafiki yangu bw. Muhammad Shafii (al-maaruf kwa Mim Shiin, ambaye hakuwa muahmadiyya) tulitoka mjini Lahore na kuelelea mjini Sargod'ha kufuata kesi ya jarida na njiani tulilala Rabwah na kuonana na khalifa Mtukufu wa Tatu alituombea dua na kusema munipe taarifa baada ya kurudi mahakamani. Anasema asubuhi tulifika mahakamani na kesi iliisha mapema ila Amir wa jimbo Pamoja na mawakili wengine walituomba mchana tule nao basi baada ya kumaliza tulipofika Rabwa nyumbani kwa Huzur kumpa marejesho baada yam chana na kugonga mlango wake mara Huzur alitufungulia mlango kana kwamba alikuwa anatungojea na kutuuliza sababu ya kuchelewa. Alipojua tulibaki pale kwa chakula cha mchana kutokana na msisitizo mkubwa basi alijibu kwamb mimi na wangu hatujapata kula tulikuwa tunakungojeni, basi mkapumzike kidogo nisali nafali za shukrani na nipate kula kisha nakuja. Bw.Saqib aalieleza kuwa yule Rafiki mim shin alposikia maneno ya khalifa na hali yake kwamba mchana ameshinda na njaa kwa ajili yetu basi hakuweza kujizuia na macho yake yalitoa machozi na alisema: nimeshajua kwa nini mnampenda khalifa wenu. Ndugu wasemaji! Ukweli ndio huu kwamba khalifa anatupenda Zaidi kuliko sisi kumpenda yeye.

Kuna **Professa mmoja** aliyekuja kutoka Canada kwa ajili ya kumtibu khalifa wan ne alipokuwa anaumwa. Yeye alisema baada ya kuonana na khalifa kwamba nilikuwa najua kuwa wanajumuiyya wanampenda sana khalifa wao lakini baada ya kuonana na khalifa nasema, khalifa wenu anawapenda Zaidi wanajumiyya.

Bibi Faiza binti yake Khalifa wa nne anaeleza kwamba siku moja Huzur alialikwa na jamaa mmoja nyumbani kwake na Huzur alikuwa anapenda sana kula Samaki kwao kwa sababu jinsi walivyokuwa wanapika kwa namna nzuri. Bi Faiza anasema tulifika kwao, tulikarbishwa kwenye chakula na mara kati ya chakula Huzur alizuia mkono wake na huzuni kubwa ilishuhudiwa usoni mwake na sisi tulishtuka kama kuna shida basi Huzur aliacha kula na kusema pigeni simu kule Pakistan kwamba kesho asubuhi Samaki wapelekwe kwa mahabusu wa Kiahmadiyya waliofungwa ndani kwa jina la Allah. Yaani kati kati ya chakula alipowakumbuka tu aliacha kula na sio hii tu bali alitoa maagizo kabisa ya kuwapelekea wale mahabusu.

Seyyedna Ahmad a.s. anasema:"Malaika na Roho Takatifu hushuka wakati ule ambamo Mtu Adhimu, Anaposhuka ardhini akivaa taji la ukhalifa na kupata maneno ya Mwenyezi Mungu. Yule khalifa hupewa roho takatifu hasa na wale malaika waliopamoja naye hushushwa kwa watu wenye bahati (nzuri).(Fathe Islam,R. KH.J.3.UK.12.Maelezo ya chini)

Lazima tuwe na uhusiano wa dhati na uaminifu mkubwa na ukhalifa ili tujifaidisha na malaika. Hazrat Musleh Maud r.a.alisema akieleza jambo hili kuwa:

"Njia moja wapo ya kujipatia baraka za malaika ni kujenga uhusiana na uaminifu kwa makhalifa waliochaguliwa na Mungu na kuwatii(makhalifa)……kuwa na uhusiano na makhalifa wa kweli kunazalisha undugu na malaika na kumjaalia mtu apate nuru za Kiungu."(Tafsire Kabir,J.2.uk.561)

Khalifa wa nne alieleza siri hii kuwa;

Ningependa kueleza kwamba nimeshashuhudia na hata mbele pia itatokea hivi kuwa, kama muahmadiyya yeyote haheshimu cheo cha ukhalifa, hampendi kikweli, na hana undugu wa moyo naye na hufika na kuhudhuria kwake kwa wakati wa shida zake tu basi maombi yake hayatapokelewa yaani maombi yake khalifa hatapokelewa kwa ajili yake(yule mtu).yatapokelewa kwa ajili ya yule tu anayemuandikia (barua) kwa uaminifu."(Al-Fazal,27 Julai 1982)

Safari moja Hadhrat Mirza Bashir Uddin Mahmood Ahmad, **khalifa wa pili** wa Seyyedna Ahmad as alisema: "Yupo mtu kwa ajili yenu, kujisikia maumivu yenu, kuwapendeni, kuzichukua shida zenu kuwa za kwake, kujaali taabu zenu kama za kwake, kuwaombeni dua kwa Mungu lakini (wapinzani) wao hawana yeyote, yeye analia mbele ya Mungu kwa ajili yenu na wao hawana. ***(Anwar ul ulum j.2.uk.156)***

Khalifa wa nne wa Seyyedna Ahmad[as] aliwahi kutuelezea hali yake kwa maneno haya kwamba: "Baadhi ya usiku ninakesha na kumlilia Mungu juu ya shida na taabu za wanajamati."

Itaendelea…. Inshallah toleo lijalo

WASIYYAH

لَنْ تَنَالُوا الْبِرَّ حَتّٰى تُنْفِقُوْا مِمَّا تُحِبُّوْنَ ۚ وَمَا تُنْفِقُوْا مِنْ شَيْءٍ فَاِنَّ اللّٰهَ بِهٖ عَلِيْمٌ ﴿۹۳﴾

Hamtaweza kuufikia wema hasa mpaka mtoe katika vile mnavyovipenda na cho chote mnachokitoa, basi hakika Mwenyezi Mungu Anakijua.(Sura Al-Imraan 3:93)

Mwenyezi Mungu anawaeleza waaminio kupitia Aya hii kuwa ili mtu aufikie wema wa kweli kabisa, basi jitihada kubwa kabisa inatakiwa kufanyika, na mtu asione kitu chochote kuwa ni kipenzi kwake isipokuwa amekitoa hicho katika njia ya Allah.

Na moja kati ya vitu ambavyo mwanadamu anavipenda zaidi ni Mali. Kwa kubainisha hilo. Qurani tukufu inaeleza kuwa

وَتُحِبُّوْنَ الْمَالَ حُبًّا جَمًّا ﴿۲۱﴾

Na ninyi mnapenda mali kwa pendo la kupita kiasi (Surat Fajr 89: 21).

Kwa hivi mwanadamu kama asingepata muongozo huo wa kumtoa katika mapenzi hayo ya kupenda mali, basi asingeliweza isipokuwa kuangukia katika huba hiyo ya kupenda mali hadi mwisho wa uhai wake.

Na kupitia Aya ya kwanza niliyoisoma yaani sura 3:93 tunapata lengo na shabaha kubwa kabisa ya kuanzishwa kwa Mpango huu wa Al-Wasiyyat. Masihi Aliyeahidiwa(a.s) alianzissha mpango huu mnamo mwaka 1905 kwa Amri ya Mwenyezi Mungu, ukiwa na lengo la kuwabaini watu waliowema kabisa wa Jumuiyya yake na waliotayari kutoa kila walichonacho kwa ajili ya Dini ya Allah.

Masih Aliyeahidiwa (a.s) katika zama za mwisho wa uhai wake, Alifunuliwa mara kwa mara na Mwenyezi Mungu juu ya kifo chake na kwa Amir ya Allah alitakiwa aandae sehemu Maalumu kwa ajili ya kuzikiwa yeye pamoja na watu hao waaminifu wa Jumuiyya yake.

Hivyo kwa shauku kubwa kabisa ililazimika aandae eneo la Makaburi alilofunuliwa na Allah kwa jina la **"Bahishti Maqbara"** yaani Makaburi ya watu wa Peponi ili yeye pamoja na watu hao waliowema kabisa wapate kuzikwa humo na ili iwe somo na kumbukumbu kwa vizazi vya baadae.

Katika kutimiza Amri hiyo Masihi Aliyeahidiwa(a.s) aliweka masharti kadhaa ili waliotayari kutimiza Masharti hayo ndio yaliobeba Mpango huu muhimu wa Al-Wasiyyat,
Na moja ya Sharti muhimu kabisa la mpango huu wa Al-Wasiyyat kama alivyoeleza Masih Aliyeahidiwa(a.s) ni kuwa
"….**miongoni mwa wanajumuiya yule tu atazikwa makaburini humu**
atakayefanya wasia ya kwamba baada ya kifo chake sehemu ya kumi ya mali atakayoacha itatumiwa kwa kueneza Islam na kuhubiri maamrisho ya Kurani sawa na maagizo ya Jumuiya hii. Na kila mkweli mwenye imani kamilifu atakuwa na hiari ya kuandika katika wasia wake zaidi yake vile vile, lakini siyo kidogo kuliko sehemu hiyo ya kumi." (Al-wasiyyat UK-23)

kupitia Sharti hili Masih Aliyeahidiwa anatoa wito kwa wale wote waliotayari kutafuta fadhila za Allah basi wafanye juhudi ya juu zaidi kutoa mali zao katika njia ya Allah kwa hatua kubwa kabisa kiasi hiki kwamba kila anachokimiliki iwe ni kipato anacho mapato, Nyumba anazozimiliki, Dhahabu, mshamba, fedha na kila aina ya mali basi sehemu yake ya kumi au kuzidi zaidi aitoa katika njia ya Allah.

Masihi Aliyeahadiwa(a.s) alitoa wito huu kwa namna ya msisitizo wa hali ya juu kabisa ili watafutao ukweli na wale wenye ikhlasi ya kweli moyoni mwao walishike jambo hili kwa uthabiti kabisa na walibebe kwa ujasili ili Allah awakubalie Kujitolea kwao kama walivyojitolea waliopita kabla yao.

Masihi Aliyeahidiwa(a.s) alieleza kuwa,
"Mwenyezi Mungu Aliweka msingi wa mtihani katika kila zama? Alitaka katika
kila zama kwamba Awapambanue wabaya na wema. Kwa hiyo, sasa pia Amefanya vivyo hivyo" (Al-Wasiyyat UK-35).

Masih Aliyeahidiwa(a.s) aliinukuu aya ya sura 29: 3 ya Qurani

اَحَسِبَ النَّاسُ اَنْ يُّتْرَكُوْٓا اَنْ يَّقُوْلُوْٓا اٰمَنَّا وَهُمْ لَا يُفْتَنُوْنَ ﴿۳﴾

Je, watu wanadhani wataachwa waseme tumeamini, nao wasijaribiwe? (surat Ankabuut 29:3)

Masihi Aliyeahidiwa(a.s) akaendelea kueleza kuwa
"Tunatambua ya kwamba kwa njia ya mtihani wa wakati huu pia watapambanuka wenye ikhlasi ya hali ya juu waliotanguliza kikweli dini juu ya dunia mbali na watu
wengine. Na itathibitika ya kwamba wametimiza ahadi ya baiati na kudhihirisha ukweli wao" (Al-Wasiyyat UK-36)

Kwa hivyo mpango huu wa Al-Wasiyyat ni jaribio kwa waaminio wa zama za leo na mwenye kuushika mpango huu kwa uthabiti na ikhlasi ya moyo na ucha-Mungu basi wametimiza Ahadi ya Masihi Aliyeahidiwa(a.s) na Allah akipenda atawalipa yaliyo ya kheri. In Shaa Allah

Hivyo shabaha ya kwanza kabisa ya nidhamu na Mpango huu wa Al-wasiyyat ni kumfanya Mwanadamu aondoe moyoni mwake ile hali ya kutawaliwa na huba ya kuvipenda vitu na mali za kidunia kutoka ndani ya nafsi yake, ambapo kama shabaha ya lengo hilo litimizwe na kila anayejiunga na mpango huu wa Al-wasiyyat alifikie lengo hilo basi hatua ya kujali na kuwahudumia viumbe wa Allah kwa huruma ya hali ya Juu kabisa itafikiwa.
Kwa Kufafanua zaidi lengo na umuhimu wa Mpango huu wa Al-Wasiyyat Khalifatul Masih II(ra) aliandika kitabu maalumu chenye maelezo na ufafanuzi wa falsafa ya Mpango huu wa Al-Wasiyyat kilichopewa jina la Nizamu Nau au New World order au Mpango Mpya wa Dunia, Huzur (ra) alieleza,

"Wakati utakuja hivi karibuni ambapo ulimwengu utalia kwa ajili ya Utaratibu Mpya. Kutoka
kila upande sauti itapazwa kutangaza Mpango Mpya. Urusi itadai kuupa ulimwengu Mpango Mpya. India itatangaza Mpango mpya. Ujerumani na Italia itatangaza Mpango mpya. Marekani itatangaza Mpango Mpya. Katika wakati huo Khalifa wa Masihi Aliyeahidiwa atatangaza kutoka Qadian: Mpango Mpya tayari umewekwa kupitia Al-Wasiyyat. Ikiwa ulimwengu unataka kupata maendeleo kwenye njia ya amani na mafanikio, njia pekee ni kuingia katika Mpango Mpya uliowekwa kwenye Al-Wasiyya"
(Nizam Nau UK-117)

Huzur(ra) akaendelea kusema kuwa;
"Mpango wa Wasiyyat utakapofikia ukomavu, hautawasaidia wabashiri tu, bali pia utasaidia kuondoa mahitaji na shida kwa kufanya utoaji wa kutosha wa mahitaji ya watu wote kama ilivyoelezwa na Uislamu. Hakuna yatima atalazimika kuomba, wala mjane hatalazimika kuomba msaada, wala mhitaji hatakiwi kupata wasiwasi. Kwa sababu Mpango wa Wasiyyat utakuwa mama kwa watoto, baba kwa vijana na chanzo cha usalama kwa wanawake. Ndugu atasamsaidia nduguye kwa hiari na upendo bila shuruti, wala hatataka malipo, kwani atapata malipo bora kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Hakuna tajiri wala masikini atakaepata hasara. Hakuna taifa litakalopigana na jingine, na baraka zake itazunguka dunia nzima"
(Nizam Nau UK-130)

Huzur(ra) akaendelea kutoa wito kwetu sisi kama wanajamaat kuwa,
"Kwa hiyo nyote mnapaswa kufanya Wasiyyat wenu chini ya

Ukurasa 04

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania

Mapenziya Mungu

MAPENZI KWA WOTE BILA CHUKI KWA YEYOTE

Ukhalifa, Uongozi bora na uliotukuka

HABARI UK> 05



HABARI UK> 8

TANGAZO

Kuelekea Ijtimaa ya Kitaifa Lajna Imaillah Tanzania

WASIYYAH

HABARI UK> 11



Al Masjid Aqsah, Qadian. Msikiti wa Sayyidna Ahmad[as]

Toeni Fatwa
Istiftaa(Urdu)
(Swahili Translation)

This book, written by Hazrat Mirza Ghulam Ahmad Qadiani[as], the Promised Messiah and Mahdi and founder of the Ahmadiyya Community in Islam, sheds light on the extraordinary circumstances that led to the fulfillment of his prophecy regarding the death of an Aryah Samāj leader, Pundit Lekhrām, who was infamous for his vituperation against the Prophet of Islam and his religion. In this small but a comprehensive book, the author has successfully argued that Lekhrām was killed as a result of the prophetic revelation the former had received from God his Lord, and which was fulfilled as a special manifestation of divine powers.
The author has also proved, with categorical arguments, that Lekhrām's murder was not a result of any conspiracy hatched on the part of the author, rather it was an event that took place in exact accord with the prophecy made in the light of divine revelation and God's extraordinary word.

ISBN 1848805484-9
9781848805484

Toeni Fatwa

Na

Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] wa Qadian

Masihi Mau'udi na Imam Mahdi

Mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya

JUMUIYA YA WAISLAMU WAAHMADIYYA
TANZANIA

Je, Wajua?

Je wajua kuwa ili uone kitu, basi mwanga unaotoka katika kile kitu unatakiwa uwe umefika machoni kwako. Mwanga wa jua unatumia dakika nane kufika duniani. Mwanga wa nyota unachukua miaka milioni kadhaa kufika duniani. Hivyo uonapo nyota, fahamu kwamba unachokiona hasa ni mwanga uliotoka katika nyota miaka milioni iliyopita, na unafika katika macho yako muda huo unaoangalia. Unachokiona sio sasa, unaona historia. Wanasayansi wanatumia historia hiyo kujua dunia iliumbwaje.

Nakala hii itapatikana kwa Tsh. 2,300/=

Kwa Makala, Maoni, Ushauri; Tuandikie

mapenziyamungu36@gmail.com